# Wote wawe na Umoja

Na Askofu Dkt. Samson Mushemba
Mkuu wa KKKT Mstaafu

Makanisa saba ya Kilutheri yaliyokuwa yameanzishwa na Wamisionari wa Ulaya na Marekani nchini Tanganyika mnamo 19 Juni 1963, yaliungana na kuunda Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanganyika (KKKT) na baadaye Tanzania. Kabla ya hapo makanisa hayo ya lihusiana kama fungamano; lakini yalipoungana yalikubaliana kuwa na Katiba moja iliyoanzisha KKKT.

Kanisa hili ni kiungo kimoja cha Yesu Kristo katika dunia nzima. Limejengwa katika misingi ya mahubiri ya manabii na mitume kama kanisa la kwanza. Kanisa la kwanza lilifanya yafuatayo ili kudumisha umoja: Kwanza lilidumu katika mafundisho ya mitume yaliyojengwa katika Neno la Mungu.

Viongozi wa kisiasa nchini wamekuwa wakitukumbusha umuhimu wa kukaa katika misingi ya umoja wetu kama taifa. Tunafahamu 'umoja ni nguvu.' Neno la Mungu ndilo lililobeba umoja na yote Mungu apendayo tuyafahamu.

Kanisa la kwanza pia lilidumu katika kusikiliza na kujifunza Neno. Mwongozo na maoni mazuri ya wachamungu yanatokana na Neno la Mungu. Washarika wanaotaka kuongozwa na kukaa katika uzima husoma Neno la Mungu kila siku wakilitafakari na linakuwa 'chakula' chao cha kila siku. Wanalisikiliza katika Ibada, mikutano ya kiroho, nk.

Mfalme Daudi alisema katika Zaburi "Neno lako ni taa ya miguu yangu na mwanga wa njia yangu". KKKT tunapokumbuka miaka 50 ya umoja; tupende kusikiliza na kulitafakari Neno la Mungu ambalo ndilo 'linaloweza kuonya na kuwabadilisha watu hasa watenda mabaya na kuwafanya wawe watu wa Mungu.'

Neno linaweza kuwabadilisha wala rushwa, wauaji, wanaochukia wenzao, wanaouza miili yao na walio na ubinafsi kiasi cha kuharibu mazingira yetu, nk. Linaweza kuwabadilisha wabadhirifu wa fedha za umma katika manispaa au halmashauri, nk. "Apendaye Neno la Mungu atakamilishwa aweze kutenda kila tendo jema," kama Paulo asemavyo.

Kanisa la kwanza lilidumu likimshuhudia Yesu Kristo aliyewaagiza: "Nanyi mtakuwa mashahidi wangu kuanzia Yerusalemu, Uyahudi yote, Galilaya na hata mwisho wa dunia." Hivyo kanisa la kwanza kwa umoja, lilimshuhudia Kristo. Mahubiri yakifuatana na uchaji; huvuta wengine wamjie Kristo na kumwamini. Kanisa la kwanza lilifuata maagizo ya Yesu kwa kudumu katika kumwomba Mungu.

Maombi yanamuunganisha Mkristo na Mungu. Na Mungu anasikia na kujibu sala za watu wake waombapo katika jina la Yesu. Bwana Yesu alisema: "Ombeni nanyi mtapewa, bisheni nanyi mtafunguliwa." Katika umoja kanisa la kwanza waliomba na walikumbuka jinsi Bwana Yesu Kristo alivyokuwa akiomba. Kuna siku aliomba usiku kucha alipotaka kuchagua mitume na pale alipokaribia kuteswa. Mitume walisinzia lakini Yesu akaendelea kuomba na aliporudi aliwauliza "mbona mmesinzia?"

Kuomba ni msingi wa uhusiano wetu na Bwana Wetu Yesu Kristo. Yesu alimwomba Mungu sana na sisi inatupasa tumwombe Mungu. Nawasihi tunapoingia kipindi hiki cha miaka mingine 50 ya umoja wa KKKT; tuingie katika kuomba hadi Yesu atakaporudi.

Tuombe Mungu atupe amani, atuondolee chuki, uadui na uhasama; si katika Kanisa tu; bali katika makanisa mengine pia. Tuombe watu wamjue Mungu na kumpenda na kumwamini Yesu Kristo aliye mkombozi wa dunia. Wakristo wakimwomba Mungu kwa imani atawasikia na kujibu sala zao.

Petro alipofungwa (Mdo 12: 5 -11); Mungu alitumia malaika wake pingu zikalegea, milango ikafunguka, Petro akatoka na alipofika chumba walimokuwamo wenzake; aliwakuta wakimwombea. Tuliombee taifa letu, watoto na jamaa zetu na tuombe umoja udumu katika Kanisa letu ili “Mungu azidishe watu wanaookolewa.” Neno la Mungu linasema “bali wote waliompokea Bwana Yesu aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu,” na hao ndio wale waliaminilo jina lake.

Wokovu wetu umetokana na Mungu kwa njia ya Yesu Kristo. Kanisa la nyakati za mitume lilikuwa likimsikia Bwana Yesu akiliombea, akifundisha, nk. Kanisa hilo lilikumbana na mateso na upinzani sana katika siku za mwanzo kutoka kwa watawala na viongozi wa dini na Wayahudi; lakini halikukata tamaa. Lilidumu katika kumpenda Bwana Yesu, likimtangaza na kumshuhudia; na Yeye akaliimarisha likashinda.

Na likawa ndio chimbuko la misioni iliyotumwa “ulimwenguni kote” kuanzia Uyahudi, Ulaya, Afrika, Asia, nk. Maombi yao yaliambatana na ushirika, kuumega mkate na kumshudia Yesu Kristo kwa nguvu na katika umoja. Na watu waliokolewa na kujiunga na kanisa. Basi ndani ya kanisa hilo Mungu akatenda maajabu makubwa na kanisa hilo linadumu mpaka sasa.

KKKT limerithi yaliyofanywa na kanisa la kwanza na maisha yake kwa sababu hayo ndiyo yanayolifanya kuwa kanisa lenye umoja na lisilo na mwisho. Utumishi na maisha ya Kanisa la Kilutheri uige mfano wa kanisa la kwanza lililoanzishwa na mitume; na ndivyo tunavyotaka iwe po pote duniani.

Mungu abariki KKKT ili liendelee kujenga utumishi na maisha yake katika msingi ulioanzishwa na Yesu. Na likifanya hivyo, litazidi kufanikiwa, kubarikiwa, kuimarika na kuweka wakristo na wafuasi wake wote katika njia iendayo kwa Bwana Wetu Yesu Kristo. Bwana Yesu Asifiwe!

(Askofu Dkt. Samson Mushemba ni Mkuu wa Kanisa Mstaafu -aliyeongoza Awamu ya Tatu).